# HAKI ZA KIBINADAMU NEW BRUNSWICK



## Je, ulifahamu kwamba New Brunswick lina sheria zakukulinda dhidi ya unyanyasaji na ubaguzi?

Ubaguzi ni unapotumiwa visivyo na mtu mwingine kwa sababu ya utofauti wako wa kitambulisho, sifa au tabia za kibinafsi, rangi, nchi ya kuzaliwa au hata hali yako kifamilia.

Kipenge cha Haki za Kibinadamu katika New Brunswick zinakulinda kimaisha dhidi ya ubaguzi kwa njia tano. Njia hizo ni; **Ajira, Makazi, Huduma, Utangazaji na Ushirika.**

Kipenge hiki kina **misingi 16 za ubaguzi.** Misingi hizi zinawakilishwa na **utambulisho** ama **sifa za kibinafsi** (kwa mfano nchi/taifa, rangi, dini) zinazoweza kuweka mtu kwa hali ya hatari ya kubaguliwa.

## Mzingi za ubaguzi ni kama:

1. **Utaifa**
2. **Rangi**
3. **Nchi ya kiasili**
4. **Pahali pa kuzaliwa**
5. **Asili ya kiukoo**
6. **Dini**
7. **Umri**
8. **Utambulisho wa Kijinsia**
9. **Ulemavu wa kimwili**
10. **Hadhi ya Ndoa**
11. **Hali ya Kifamailia**
12. **Jinsia (hadi ya ujauzito)**
13. **Mwelekeo wa kingono**
14. **Utambulisho wa Kijinsia**
15. **Hali ya Kijamii**
16. **Madili za kisiasa**

Kipenge, kwazaidi hulinda kutokana na **unyayasaji wa kimapenzi** au **ngono na kulipiza kisasi** (yaani unapotendewa vibaya kwa sababu uliwasilisha malalamishi ya haki ya kibinadamu ama ulisaidia na malalamiko yaliopo.)

## Kwa mfano, kipenge hiki hulinda kutokana na ubaguzi:

- Unapopanga nyumba (**Makazi**);
- Unapofanya ununuzi ama kula katika mkahawa (**huduma**);
- Unapoenda shule/masomoni (**huduma**);
- Unapotafuta kazi ama mahojiano za ajira (**Ajira**);
- Ukiwa mwanachama wa shirika fulani la umoja (**ushirika wa kibiashara**);

## Wajibu wa kuzingatiwa



Unapokuwa na mahitaji, mwajiri wako (mwenye nyumba ama mhudumu) lazima **azingatie** kwa busara matakwa ama mahitaji yako. Hili linaitwa **wajibu wa kuzingatiwa na lipo kwenye sheria.**

**Kwa mfano:**
Unaposhughulikia mwana wa familia yako anayeugua kutokana na gonjwa sugu (**hali ya kifamilia**) na unahitaji ruhusa ili umpeleke kuona daktari kila wiki. Mwajiri wako ana **wajibu wa kuzingatia** ratiba yako ya kazi ili uweze kutekeleza mahitaji zako za kimalezi.

## Zaidi juu ya Wajibu wa kuzingatiwa

**Wajibu wa kuzingatiwa** unamaanisha kwamba waajiri, wenye nyumba za kupanga ama wahudumu hawafai kubadilisha sheria na masharti ili kukinga binadamu kutokana na ubaguzi dhidi ya wanaolindwa na kipenge hiki.

Ikiwa ngumu kwa mwajiri kuwajibika na kutozingatia matakwa ya anayelindwa na kipenge hiki (kwa sababu ya usalama) huenda watakosa kuwajibika LAKINI sio kwa lazima. Huu unaitwa ugumu usiyofaa.



## Mifano za Ubaguzi

**Ubaguzi unaotoka na na rangi au asili ya kiukoomka tika utoaji wa huduma:**
Tao ni mwanafunzi wa shule ya upili. (**Huduma**)Mwalimu wake wa sayansi humchagua kila mara na kutoa maoni juu ya urithi wake ya Ki-Asia. (**rangi au asili ya kiukoo**). Tao huwa na wasiwasi na kufikiria kwamba mwalimu anaeneza ubaguzi darasani.

**Ubaguzi unaotokana na hadhi ya familia katika upangaji wa nyumba:**
Juan anaishi katika nyumba ya gorofa (**upangaji**)na mweke na wanapata mtoto mchanga(**hadhi ya familia**). Juan anapojulisha mwenye nyumba kuwa kuna mabadiliko kwa familia yake, anaambiwa ahame kwa sababu makazi yale ni ya watu wazima.

**baguzi unaotokana na ulemavu wa kiakili katika utoaji wa huduma:**
Jacques hutegemea **huduma** za wanyama kwa **ulemavu** wake wa kiakili na anakwenda sokoni. Pale dukani meneja anamwambia kuwa hawezi kuingia mahali pale na mbwa wake. Jacques anawaeleza kuwa mbwa huyo ni mnyama mhudumu lakini bado anakatazwa kuingia dukani.

**Kulipiza kisasi katika ajira:**
Imani ni mfanyi kazi wa muda katika nchi ya kigeni na anahudumu kwa mkahawa (**ajira**). Analeta malalamishi za haki za kibinadamu kwamba mwajiri wake anatoa maoni yasiyofaa kwa wafanyi kazi wa kike. Mwajiri wake anapogundua kuna malalamishi dhidi yake anamfuta Jacques kazi (**kisasi**) na kujulisha waajiri wenzake walio karibu wasimwajiri.

## Jinsi ya kufanya unapobaguliwa

**Tume ya haki za kibinadamu ya New Brunswick** ni shirika la serikali linalohakikisha kuwa haki za wakazi wa New Brunswick zimelindwa chini ya kipenge hiki. Tume hutoa **ujumbe za bure** kuhusu haki kza kibinadamu na kusaidia wanaobaguliwa katika katika New Brunswick.

Ikiwa unahisi kubaguliwa unaweza peleka **malalamishi** yako kwa tume. Tume hili hutumia njia zinazofuata **utaratibu**.

## Kuleta malalamishi kwa Tume, tunapendekeza:

1. Kwanza **wasiliana na Tume** ili kujadili hali ya mambo na kupata ujumbe kuhuzu kipenge hiki na **taratibu zinazofuatwa**. Majadiliano haya yatabaki kuwa siri mpaka uamue kupeleka malalamishi yako mbele ya Tume.

2. **Jaza fomu ya malalamishi.** Fomu hizi hupatikana katika mtandao wa Tume. Pia unawezatumiwa fomu kupitia barua pepe. Jaza sehemu zote ukisimulia tukio kwa njia bora zaidi uwezekanavyo. Mwanafamilia, rafiki ama wakili anaweza kukusaidia kujaza fomu. Wanaweza kukuwakilisha katika harakati zote lakini lazima Tume lijuishwe.

3. **Husika katika utaratibu zinazofuatwa.** Baada ya kuwakilisha malalamishi Tume litawasiliana nawe kila mara kujua utaratibu wa malalamishi umefika wapi. Unaweza wasiliana na Tume kwa wakati wowote unapokua na swali lolote kuhusiana na malalamishi yako.

## Wasiliana nasi kwa:


(506) 453-2301

hrc.cdp@gnb.ca

www.gnb.ca/hrc-cdp